

VEDLEGG: VEILEDER TIL NORSKPLAN

## **Maelezo kuhusu mpango wa kinorway kwako wewe ambaye utahudhuria elimu ya lugha na elimu jamii.**

### **Kuhusu mpango wako wa lugha**

- Wewe pamoja na manispaa yako mtashirikiana kutengeneza mpangokazi wa majifunzo ya lugha na elimujamii. Elimu hii itasaidia katika kujifunza lugha vizuri, elimu ya jamii ya Norway, na pia uweze kupata kiunganishi cha kuwa na maisha ya kufanya kazi ya kudumu.

### **Norskmål**

- Wanafunzi wa lugha ya kinorwej wanapaswa kufuzu kiwango cha chini cha lugha. Manispaa na mkoa watawajibika na kuhakikisha kwamba mwanafunzi anafuzu kiwango cha chini cha lugha. Kiwango cha chini kinakidhi vigezo vya malengo yanayomuhusu mwanafunzi wa lugha.

### **Ukomo na upana wa elimu**

- Watu wote wenye vibali vya kuishi hapa nchini vinavyowapatia haki na wajibu wa kuingia katika masomo ya kinorwej na elimu ya jamii wanapaswa kuendelea na masomo hadi wafikie daraja la chini la lugha, yenye kumaanisha utimilifu wa malengo ya lugha ya kinorwej. Hata hivyo, muda wa elimu hauwezi kuzidishwa miaka mitatu pamoja na kupatiwa kibali maalumu cha kufanya hivyo.
- Mwanafunzi ambaye alimaliza masomo ya sekondari ya juu, au ameshahudhuria chuo cha elimu ya juu hana haki wala hawajibiki kusoma zaidi ya miezi 18 na nyongeza ya muda kwa kibali maalumu.
- Wale ambao wanawajibika kusoma lugha na elimu ya jamii wana wajibu wa kusoma mpaka wafikie daraja la chini(lengo la wanafuzi la lugha) au hadi watimize masaa 300 ya kujifunza lugha.
- Somo la elimu ya jamii litafundishwa kwa lugha ile ambayo mwanafunzi anaelewa vizuri. Masomo yatatolewa ndani ya mwaka wa kwanza mara tu haki na wajibu vinapotolewa. Hii si lazima ikiwa elimu ya jamii inatolewa na mamlaka ya mkoa.

### **Kutokuhudhuria na Utoaji wa rufusa**

Unaweza ukaomba rufusa usihudhurie katika majifunzo ya lugha na elimu ya jamii kwa mamlaka ya mmanispaa. (Waweza kuona andiko pekee kuhusiana na hayo katika sheria na kanuni zilizopo [www.imdi.no](http://www.imdi.no) )

### **Kufukuzwa shule**

- Manispaa yaweza kutoa uamuzi wa kumfukuza mwanafunzi shule moja kwa moja ikiwa kuna sababu za kutosha za kufanya hivyo kwa

mwanafunzi mhusika. Visababishi vya kufukuzwa shule vyaweza kuwa kama vile utoro uliokithiri, tabia inayoweza kuleta athari hasi kwa mwanafunzi mwenyewe au wanafunzi wengine zinazoweza kusababisha wasimalize msomo yao, au kwa sababu ya ugonjwa wa muda mrefu.

### **Mitihani**

- Wanafunzi wenye vibali vinavyoruhusu na kuwajibisha kuhudhuria masomo ya lugha na elimu ya jamii wanapaswa kufanya mtihani wa mwisho wa lugha na wa elimu ya jamii.
- Wajibu huo hauwahusu wale wanafunzi ambao wameruhusiwa kwa kibali maalumu. Kibali hiki kinapatikana kwa njia ya mwanafunzi kuomba asifanye mitihani, manispaa inawajibika kushughulikia maombi hayo kwa kutumia sheria na kanuni zilizowekwa.
- Mtihani wa mwisho wa masomo ya elimu ya jamii unapaswa kufanywa katika kipindi cha mwaka ule ambao mwanafunzi alipewa haki na wajibu wa kuingia shuleni. (Kanuni hii haihusiki pale ambapo mamlaka ya mkoa ndiyo inatoa elimu ya jamii).
- Manispaa itahakikisha kwamba wanafunzi wenye haki na wajibu wa kufanya mitihani ya lugha na ya elimu ya jamii wanapewa nafasi ya kufanya hivyo.

### **Ungependa kulalamikia mpango huu wa kujifunza lugha?**

- Unaweza kulalamikia kuhusu masomo na mafundisho yaliyomo katika mpango wako wa kujifunza lugha

*Ikiwa unataka kutuma malalamiko yako fanya yafuatayo:*

- Peleka malalamiko yako kabla ya majuma matatu hayajapita tangu upatiwe maelezo yanayohusu mpango wa kujifunza lugha.
- Peleka malalamiko yako kwa kitengo cha manispaa kilichotoa maamuzi unayolalamikia kuhusu mpango wa kujifunza lugha
- Andika unacholalamikia
- Lazima utie sahihi/saini yako

Unaweza kutuma malalamiko yako kupitia kwa muwakilishi wako. Muwakilishi wako atakubalika pale tu ambapo atakuwa na barua ya maandishi ya kuthibitishwa nawe. Barua ya uthibitisho ni lazima ioneshe kile ambacho muwakilishi wako anapaswa kukifanya kwa niaba yako wewe. Ikiwa una mwanasheria basi huhitaji kumpatia barua ya uthibitisho.

### **Maelezo zaidi kuhusu mpango wa ujumuishwaji yanapatikana wapi?**

Maelezo zaidi kuhusu mpango wa ujumuishwaji waweza kuyapata katika sheria ya ujumuishwaji wa jamii. Sheria na kanuni zake inapatikana [www.imdi.no](http://www.imdi.no) na [Kompetanse Norge nettsider](http://Kompetanse Norge nettsider).

Kila la kheri katika masomo yako!